

Toleo 27 - Rajab 1440 H / April 2019 Miladi



Utafutaji wa Shahada

**Mzozo wa Bahari
Kati ya Kenya na
Somalia**

**Sifa muhimu za
Mbebaji Da'wah**

**Sababu za Kuvunjika
kwa Familia**

**Njia ya Mtume (saw)
Kuleta Mageuzi -
Halaqa 21**

**SWALI/JAWABU:
Ukweli wa Kura
ya Maoni ya Mradi
wa Kujitoa kwa
Uingereza**



**Khilafah
Mlinzi Wangu! Ngao Yangu!**



الله اکبر
لَا إِلَهَ إِلَّا
اللهُ
حَمْدُهُ
كُلُّ
الْحَمْدٍ

KHILAFAH

Mlinzi Wangu! Ngao Yangu!

#Khilafah_MyGuardian_MyShield



WOMENANDSHARIAH



@WOMENFORKHILAFAH



@WOMENSHARIA

Mwezi wa Rajab unatukumbusha tukio baya mno zaidi ya miaka 90 iliyopita pale ambapo dola adhimu, uongozi wa Kiislamu, Nidhamu ya Mwenyezi Mungu (swt), Khilafah ilivunjwa kwa mikono ya Magharibi wakoloni na vibaraka wao katika ardhi za Waislamu. Na kwa tukio hilo, Ummah wa Waislamu ulipoteza Mlinzi na Ngao na kudidimizwa katika muhula uliojaa kiza kinene cha kihistoria.

Kwa miongo kadhaa ikiwa sio karne, serikali za Kimaghribi na vyombo vya habari na taasisi za kisekula pamoja na serikali vibaraka zilizoko ndani ya ardhi za Waislamu zimejaribu kupaka matope fikra ya Khilafah na kuioneshwa kirongo kuwa eti ni dola ya ukandamizaji, kigaidi, kihayawani, iliyoko nyuma na kikwazo kwa wanawake. Lakini si kweli! Kinyume chake ni nidhamu iliyoomrisha na Mwenyezi Mungu (swt) ili kutawala dola. Ni njia za kufikia haki, usalama na ustawi kwa ardhi zetu. Ni muwakilishi na mtetezi wa Dini yetu. Inasimamia maslahi yetu kama Waislamu. Na ni mlinzi wa mambo yetu na mkidhiaji mahitaji yetu!

Rajab hii, Kitengo cha Wanawake Katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir itaendesha kampeni kwa kichwa "Khilafah: Mlinzi Wangu! Ngao Yangu!" ambayo itawasilisha ruwaza ya namna gani Khilafah Rashidah iliyosimama kwa njia ya Utume, ilio na misingi, sheria na nidhamu za kusuluhiha kivitendo matatizo yetu kama wanawake Waislamu na kuhakikisha ulinzi kwa maisha, mali, heshima na imani yetu. Hili limeelezewa kwa upana katika vitabu na kielelezo cha katiba vya Hizb ut Tahrir ambavyo vimeelezea kwa ukamilifu namna jinsi gani dola hii adhimu itakavyofanya kazi na kusimamia mahitaji na maslahi ya watu wake na Uislamu.

Tunawalingania kwa moyo mkunjufu muweze kufuatilia na kuinusuru kampeni hii muhimu na mujiunge na dori hii muhimu ya kuleta mabadiliko ya kusimamisha Serikali adhimu ya Khilafah ambayo itabeba jukumu kubwa la Dini yetu ndani ya ardhi za Waislamu na kuitia kwake Ummah huu utapata hadhi, haki na ulinzi.

#Khilafah_MyGuardian_MyShield

Utafutaji wa Shahada (Kifo katika Jihadi)

Utafutaji wa shahada imekuwa daima ni fahamu msingi ndani ya elimu ya kijeshi enzi za Uislamu. Pamoja na masomo juu ya zana za vita, mikakati na mbinu, utafutaji wa shahada ulitizamwa kama msingi wa fahamu za masomo, uelewaji na ujengaji wa nafsiyya. Utafutaji wa shahada ndio ultiotia nishati majeshi ya Kiislamu katika vita, ukiwawezesha kufikia yale ambayo wengine walishindwa kuyafikia na wasingejaribu kuyafikia. Huku majenerali wa majeshi ya makafiri wakiwa wamejifunga na dunia, wakipanga mikakati yao kuhakikisha kuna majeraha kidogo, majenerali wa majeshi ya Kiislamu walikuwa wamebarikiwa wanajeshi ambaa waliona kifo katika uwanja wa vita kama mlango wa kupata zawadi kubwa kwa roho yoyote inayotaka.

Utafutaji wa shahada uliwaruhusu wanajeshi Waislamu kusimama kidete pasi na wasiwasi wowote dhidi ya majeshi makubwa ukilinganisha idadi yao na kuyashinda baadaye. Maafisa wa enzi za Kiislamu hawakuchukulia kufanya kazi ndani ya vikosi nya jeshi kama njia ya kupata ajira, usafiri, nyumba na elimu kwa watoto wao kama ilivyo sasa kwa maafisa wa vikosi nya jeshi ndani ya dola za Waislamu leo. La, macho yao daima yalikuwa yamefungika tu kwa zawadi kubwa ya milele ambayo hawawezi kuipata duniani humu wanamoishi tena kwa muda mfupi.

Katika zama zetu, baada ya kuangushwa utawala wa Kiislamu, matamanio ya Waislamu ya utafutaji shahada yanaendelea kuwatia tumbo joto wanamikakati wa majeshi ya Kimagharibi na kuwakatisha tamaa. Msukumo wa kufikia shahada unaangaliwa kama uboreshaji wa kikosi ki aina yake. Umewaruhusu Waislamu pasi na kuwa na kikosi cha jeshi kilichoandaliwa vyema kuweza kupeana kipigo na kuyatia hasara kubwa majeshi ya kiuvamizi kama inavyoonekana ndani ya Afghanistan na Kashmir. Imewalazimisha Wamaghari kusoma kwa makini somo la mbinu za kivita zisizokuwa kawaida, ambazo zimewashangaza kumuona mwajeshi Muislamu akitamani shahada. Na kuwatia uoga wakuu mionganoni mwa Wamaghari kila wanapofikiria uunganishwaji wa vikosi nya majeshi ya Waislamu dhidi yao, ambalo ni jambo lisiloepukika kutokana na kurudi tena kwa Khilafah kwa Njia ya Utume.

Utafutaji shahada ni fahamu msingi ndani ya Uislamu na ambayo inaelezea sifa za Ummah wa Uislamu. Mwenyezi Mungu (swt) Asema:

وَلَا تَحْسِبَنَّ الَّذِينَ قُتُلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ - فَرَحِينٌ بِمَا عَانَهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَيَسْتَبِشُونَ بِالَّذِينَ لَمْ يُلْحَقُوْا بِهِمْ مِنْ خَفِيفٍ أَلَا خَوْفٍ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَخْرُقُونَ

“Wala kabisa usiwadhanie walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi. Wanafurahia

aliyo wapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila yake, na wanawashangilia wale ambaa bado hawajajiunga nao, walio nyuma yao, ya kwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawata huzunika.” [Aali Imran 3:169-170].

Hapa Mwenyezi Mungu (swt) Anasema kwa yakini kuwa licha ya kwamba mashahidi wameuawa katika maisha haya, roho zao ziko hai na zinaendelea kupokea mahitaji yao Katika Maisha ya Milele. Katika Sahihi Muslim amerikodi kuwa Masruq alisema, “Tulimuuliza `Abdullah kuhusiana na Ayah hii,

وَلَا تَحْسِبَنَّ الَّذِينَ قُتُلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ
“Wala kabisa usiwadhanie walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi.”

Alisema tulimuuliza RasulAllah (saw) suali hilo hilo na (saw) alisema:

أَرْوَاحُهُمْ فِي جَوْفِ طَيْرٍ خَضْرٍ، لَهَا قَنَادِيلٌ مَعْلَقَةٌ بِالْعَرْشِ، تَسْرُحُ مِنَ الْجَنَّةِ حَيْثُ شَاءَتْ، ثُمَّ تَأْوِي إِلَى تِلْكَ الْقَنَادِيلِ، فَاطْلَعَ إِلَيْهِمْ رَبُّهُمْ أَطْلَاعَةً فَقَالَ: هُنَّ شَتَّهُونَ شَيْئًا؟ قَالُوا: أَيْ شَيْءٍ نَشَّهِي وَنَحْنُ نَسْرَحُ مِنَ الْجَنَّةِ حَيْثُ شَيْئًا؟ فَفَعَلَ ذَلِكَ بِهِمْ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ، فَلَمَّا رَأَوْا أَنَّهُمْ لَنْ يَنْتَهُوا مِنْ أَنْ يَسْأَلُوا، قَالُوا: يَا رَبَّنَا إِنَّنَا نَرَدَ أَرْوَاحَنَا فِي أَجْسَادِنَا حَتَّى نُقْتَلُ فِي سَبِيلِكَ مَرَّةً أُخْرَى، فَلَمَّا رَأَى أَنَّ لَيْسَ لَهُمْ حَاجَةً، تَرَكُوا

“Roho zao zimo ndani ya ndege wa kijani ambaa wana taa, ambazo zinalewalewa chini ya Arshi ya Mwenyezi Mungu, na wanazunguka ndani ya Pepo popote wanapotaka. Kisha wanarudi katika taa hizo. Mwenyezi Mungu huwatizama na kusema, ‘Je mnatamani chochote?’ Wao husema, ‘Tutamani kipi zaidi, wakati tunatembea popote tunapotamani ndani ya Pepo.’ Mwenyezi Mungu akawauliza tena suali hili mara tatu, na walipoona kwamba Ataendelea kuwaliza mpaka watoe jibu, wakasema, ‘Ewe Mwenyezi Mungu! Tunatamani roho zetu zirudishwe katika miili yetu ili tuuliwe tena kwa ajili Yako.’ Mwenyezi Mungu alijua hawana matamanio mengine, kisha wakawachwa.”

Kwa hiyo ni muhimu kwa afisaa Muislamu kutafakari cheo cha ndugu yake mwajeshi aliyepata shahada akiwa Uhud. Autafakari kwa kina ujumbe waliomuachia miaka yote hiyo. Imam Ahmad alirekodi kuwa Ibn `Abbas alisema kuwa Mtume (saw) alisema,

لَمَّا أُصِيبَ أَخْوَانَكُمْ بِأَذْبَحَ، جَعَلَ اللَّهُ أَرْوَاحَهُمْ فِي أَجْوَافِ طَيْرٍ خَضْرٍ، تَرَدَّ أَنْهَارُ الْجَنَّةِ، وَتَأَكَّلَ مِنْ ثَمَارِهَا، وَتَأْوِي إِلَى قَنَادِيلٍ مَنْ ذَهَبَ فِي ظِلِّ الْعَرْشِ، فَلَمَّا وَجَدُوا طَبَبَ مَشْرِبَهُمْ وَمَأْكُولَهُمْ، وَحَسْنَ مُنْقَبَّهُمْ قَالُوا: يَا لَيْلَتُ أَخْوَانَنَا يَعْلَمُونَ مَا صَنَعَ اللَّهُ لَنَا، لِنَلَا يَرْهُدُوا فِي الْجَهَادِ، وَلَا يَنْكُلُوا عَنِ الْحَرْبِ، فَقَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: أَنَا أَلْيَهُمْ عَذْمَ

“Ndugu zenu walipouliwa katika Uhud, Mwenyezi Mungu aliziveka roho zao ndani ya ndege wa kijani walioeleke katika mito ya Pepo na kula kutoka

Endelea Uk..4

katika matunda yake. Kisha wanarudi katika taa za dhahadu zinazolewalewa katika kivuli cha Arshi. Walipoonja utamu wa chakula chao, vinywaji na makaazi yao, walisema kuwa, ‘Tunatamani ndugu zetu wangelijua yale ambayo Mwenyezi Mungu aliyoleta ili wasiweze kuachana na Jihadi au vita.’ Mwenyezi Mungu alisema, ‘Nitawafikishia habari zenu.’

Mwenyezi Mungu akateremsha Ayah ifuatayo:

وَلَا تَحْسِبَنَّ الَّذِينَ قُتُلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَخْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ
“Wala kabisa usiwadhanie walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi.”

Hivyo basi, afisaa wa enzi ya Kiislamu alikuwa si tu ana hamu ya malipo ya Tahajjud na kuswali Msikitini, alikuwa Analia na huku silaha yake ikiwa mikononi mwake madhubuti huku akiomba Dua, akitamani kupata shahada. Hakika, dua ya afisaa Muislamu au mwajeshi sio tu kwa ajili ya majumba, magari na elimu nzuri bali ni kwa ajili ya shahada. Mu'adh bin Jabal (ra), mwanamikakati shupavu aliyemshauri RasulAllah (saw) katika Vita vya Badr, alisimulia kuwa RasulAllah (saw) alisema,

مَنْ سَأَلَ اللَّهَ الْفَتْنَةَ فِي سَبِيلِهِ صَادِقًا مِنْ قَبْلِهِ أَعْطَاهُ اللَّهُ أَجْرَ الشَّهِيدِ
“Yeyote anayemuomba Mwenyezi Mungu ili auliwe katika njia Yake kwa dhati kutoka moyoni, Mwenyezi Mungu atampa zawadi ya shahada.” [Tirmidhi].

Afisaa Muislamu hajali hadhi wala cheo katika dunia hii lakini anatafuta hadhi ya shahada na cheo kinachotokana nayo. Imamu Ahmad alirekodi kuwa Anas alisema kuwa RasulAllah (saw) alisema:

مَا مِنْ نَفْسٍ تَمُوتُ، لَهَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ، يَسْرُّهَا أَنْ تَرْجِعَ إِلَى الدُّنْيَا، إِلَّا الشَّهِيدُ، فَإِنَّهُ يَسْرُّهُ أَنْ يَرْجِعَ إِلَى الدُّنْيَا فَيُقْتَلَ مَرَّةً أُخْرَى، لِمَا يَرَى مِنْ فَضْلِ الشَّهَادَةِ
“Hakuna roho ambayo imeridhiwa na Mwenyezi Mungu na ikafa itatamani kurudi katika maisha haya, isipokuwa ya shahidi. Atatamani kurudishwa katika maisha haya ili aweze kuuliwa tena, ili aweze kuonja cheo cha kupata shahada.”

Shahada ni kitendo kimoja ambacho kitamfanya mtu kutamani kutoka Jannah kwa fursa ya kufa tena na wakati utajiri wa dunia nzima utakapajaribu kumzua utashindwa. Imesimuliwa kutoka kwa Anas b. Malik RasulAllah (saw) alisema,

مَا مِنْ أَحَدٍ يَدْخُلُ الْجَنَّةَ يُحِبُّ أَنْ يَرْجِعَ إِلَى الدُّنْيَا وَأَنَّ لَهُ مَا عَلَى الْأَرْضِ مِنْ شَيْءٍ بَعْدِ الشَّهِيدِ فَإِنَّهُ يَتَمَّنِي أَنْ يَرْجِعَ فَيُقْتَلَ عَشْرَ مَرَّاتٍ لِمَا يَرَى مِنَ الْكَرَامَةِ
“Hakuna atakayeingia Peponi atatamani kurudishwa tena duniani lau hata angelipewa kila kitu juu ya mgongo wa ardhi (kama kishajiisho) isipokuwa shahidi ndiye atakayetamani kurudishwa tena katika ardhi hii na auliwe mara kumi kwa ajili ya cheo kitukufu ambacho amepewa.” [Muslim]

Afisaa Muislamu hayafungi macho yake juu ya kuwapa umadhubuti wa kifedha familia yake bali anakwenda mbio kuwafungulia njia ya kuingia Jannah, iliyojaa mazuri yasiyokuwa na mwisho. Imesimuliwa na Abu al-Darda', RasulAllah (saw) alisema,

يُشَفَّعُ الشَّهِيدُ فِي سَبْعِينِ مِنْ أَهْلِ بَيْتِهِ

“Shahid atapewa nafasi kuwaombea watu sabini wa familia yake.” [Abu Dawud].

Afisaa Muislamu haendi mbio kuchuma mali nydingi ambazo wanaomtegomea waweze kustarehe nazo baada ya kifo chake, kwa kuwa anajua kuwa shahada ni manufaa makubwa kwa wanaomtegomea. Abu Bakr Ibn Marduyah amerekodi kuwa Jabir bin 'Abdullah alisema, “Mtume wa Mwenyezi Mungu aliniangalia siku moja na akasema, ‘Ewe Jabir! Kwa nini nakuona una majonzi?’ Nikasema, ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Babangu alipata shahada na kuniachia madeni na watoto.’ Akasema,

إِلَّا أَحْيِرُكُ؟ مَا كَلَمَ اللَّهُ أَحَدًا قُطُّ إِلَّا مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ، وَإِنَّهُ كَلَمَ أَبْنَاكَ كَفَاحًا
سَلَّنِي أَعْطَكَ، قَالَ أَسْأَلُكَ أَنْ أُرْدَ إِلَى الدُّنْيَا فَأَقْتَلَ فِيكَ ثَانِيَةً، فَقَالَ الرَّبُّ عَزَّ وَجَلَّ
إِنَّهُ قَدْ سَبَقَ مِنِّي الْقَوْلُ إِنَّهُمْ إِلَيْهَا لَا يَرْجِعُونَ. قَالَ أَيُّ رَبٍ فَأَبْلِغْ مَنْ وَرَأَيَ

“Nikwambie kuwa Mwenyezi Mungu hakuwahi kuzungumza na yejote isipokuwa nyuma ya pazia. Lakini, Alizungumza na babako moja kwa moja.” Akasema, ‘Niombe na Nitakupa.’ Akasema, ‘Naomba nirudishwe hai ili ni ubiwe katika njia Yako tena.’ Mwenyezi Mungu, Aliyetakasika, akasema, ‘Nimezungumza neno kuwa hawatorudishwa tena katika (haya maisha).’ Akasema, ‘Ewe Mwenyezi Mungu! Basi nifikishie habari zangu kwa nilio wawacha nyuma.’

Afisaa Muislamu yuko makini na sehemu yake ya mwisho, uchungu wa kifo, adhabu ya kaburi na uoga wa kupindukia unaotokana na kutosamehewa Siku ya Hesabu. Kwa hiyo anatzama fadhila tukufu za Mwenyezi Mungu (swt) zinazotokamana na shahada. Imesimuliwa kutoka kwa Abu Hurairah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (swt) alisema,

مَا يَجِدُ الشَّهِيدُ مَسْأَلَةً لِمَنْ قُتِلَ إِلَّا كَمَا يَجِدُ أَحَدُكُمْ مَسَأَلَةً لِفَرَصَةٍ

“Shahidi hahisi kitu chochote anapouliwa zaidi ya mmoja wenu anavyohisi anapoumwa na (chungu).” [Ibn Majah]

Imesimuliwa kutoka kwa Rashid bin Sa'd, kwamba mwanamume mmoja mionganii mwa Maswahaba wa Mtume alisema, “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa nini waumini watapewa mitihani katika makaburi yao isipokuwa shahidi? Mtume (saw) alisema,

كُفَىٰ بِبَارَقَةِ السُّبُّوْفِ عَلَىٰ رَأْسِهِ فَشَّةٌ

“Kupambana kwa panga juu ya kichwa chake ni mtihani tosha.” [an-Nisai].

Mtume (saw) alisema,

يُعْفَرُ لِلشَّهِيدِ كُلُّ ذَنْبٍ إِلَّا الدِّينَ

"Mwenyezi Mungu humsamehe kila dhambi shahidi, isipokuwa deni lake." [Muslim].

Na imesimuliwa kutoka kwa Miqdam bin Ma'dikarib kwamba Mtume (saw) alisema,

لِلشَّهِيدِ إِنَّ اللَّهَ سَيِّدُ الْخَصَالِ يُعْفَرُ لَهُ فِي أَوَّلِ دَفْعَةٍ مِّنْ دَمِهِ وَيُرِيَ مَقْعِدَهُ مِنَ الْجَنَّةِ وَيُجَازَ مِنْ عَذَابِ الْفَقِيرِ وَيَأْمُنُ مِنَ الْفَرْعَانِ وَيُحَكَى حَلَةُ الْإِيمَانِ وَيُرَوَّجُ مِنَ الْخُورِ الْعَيْنِ وَيُشَفَّعُ فِي سَبْعِينِ إِنْسَانًا مِّنْ أَقْرَبِهِ

"Shahidi ana mambo sita (amewekewa) na Mwenyezi Mungu: Ana samehewa kuanzia kudondoka kwa tone la damu yake inapomwagwa; anaonyeshwa sehemu yake ndani ya Pepo; ana epushwa na adhabu za kaburi; ana wekwa salama na Hofu Kubwa, ana vishwa vazi la imani; ana ozeshwa (wake) miongoni mwa wenye macho mapana; na anaruhusiwa kuwaombea watu sabini wa familia yake." [Ibn Majah].

Na Afisaa Muislamu wa kuigwa, kusifiwa na kuonewa vivu ni yule ambaye sifa yake imejengwa na Uislamu, na kilele chake ni moto wa matamano ya kupata shahada. Kwa hiyo, lazima ayatafakari maneno ya Umar al-Faroop (ra) aliyechagua majenerali baada ya majenerali waliopata ushindi baada ya ushindi. Imamu Malik amesimulia kutoka kwa Yahya ibn Saeed kuwa Umar ibn al-Khattab (ra) alisema,

كَرَمُ الْمُؤْمِنِ تَقْوَاهُ وَيَئُونَهُ حَسْبُهُ وَمَرْوِعَتُهُ خَلْقُهُ وَالْجُرْأَةُ وَالْجُنُونُ يَضْسُدُهَا اللَّهُ حَيْثُ شَاءَ فَالْجَبَانُ يَغْرِي عَنْ أَبِيهِ وَأُمِّهِ وَالْجُرْيَةُ يُفَاقِدُهُ عَمَّا لَا يَوْبُ بِهِ إِلَى رَحْلِهِ وَالْقُلْنُ حَفَقَ مِنَ الْحَنْوُفِ وَالشَّهِيدُ مِنْ احْسَبَ نَفْسَهُ عَلَى اللَّهِ

"Utukufu wa Mu'min ni uchajimungu. Dini yake ndiyo ukoo wake. Uume wake ni katika tabia yake nzuri. Ujasiri na uoga ni ghariza ambazo Mwenyezi Mungu ameziweka pale Anapotaka. Muoga ni yule ambaye ana shindwa hata kumtetea babake na mamake, na jasiri ni yule anayepigana kwa ajili ya vita sio ngawira. Kuuliwa ni njia moja ya kukutana na kifo, na shahidi ni yule anayejitoa muhanga akitarajia zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu." [Muwatta]

Ni starehe na fadhila aina gani zilizoko mbele ya Afisaa Muislamu anayetafuta shahada! Nyuma yake ni kudhilalishwa kwa Ummah huu mikononi mwa makafiri katika ardhi za karibu na mbali, Ardhi Tukufu –Palestina, Afghanistan, Kashmiri, Myanmar (Burma), Syria, Mashariki Turkestan na Iraq. Kati yake na shahada ni kurudisha tena enzi ya Kiislamu wakati ambapo simba kwa mara nyingine watafunguliwa na kuachwa kuwashughulikia maadui waoga, ambao watakimbia kama fisi kama walivyofanya kabla yao. Na kwa dharura iliyoko mbele yake ni kutoa Nussrah yake ili kusimamisha tena Khilafah kwa Njia ya Mtume (saw) ili aweze kupata moja kati ya Husnain, ushindi au shahada.

Musab Umair – Pakistan

Habari & Maoni

Mzozo wa Bahari Kati ya Kenya na Somalia: Mzozo wa Kikoloni Kuhifadhi Maslahi ya Mabwana Wamagharibi

Habari

Mzozo wa eneo katika Bahari ya Hindi kati ya Kenya na Somalia umezidi moto baada ya Nairobi kuamua kukata mahusiano ya kidiplomasia na Mogadishu kwa sababu ya madai kuwa Somalia imepiga mnada maeno ya mafuta yaliyoko katika eneo la mzozo. Eneo lilopo katika mzozo ni mraba mwembamba katika Bahari ya Hindi uliyo na urefu wa maili 62,000. (standardmedia.co.ke)

Maoni

Serikali Kuu ya Somalia iliyoko Mogadishu na inayoongozwa na Mohamed Abdullahi Mohamed "Farmajo" imiegemea Marekani. Tangu Farmajo alipoingia mamlakani mnamo 16 Februari 2017, utawala wake umekuwa ukipata upinzani kutoka kwa Majimbo wanachama wa Somalia yanaoegemea Uingereza na yakiongozwa Ahmed Mohamed Islam "Sheikh Ahmed Madobe" ambaye ndiye kiongozi/rais

wa Jimbo la Jubaland nchini Somalia ambao mjini wake ni Kismayo. Viongozi hao wanaoegemea Uingereza waliandaa mukutano wao wa kwanza mnamo Oktoba 2017 na mukutano wa pili mnamo Septemba 2018 ambao ulihudhuriwa na marais – Abdiweli Mohamed Ali Gaas (Puntland), Ahmed Duale Gelle (Galmudug), Mohamed Abdi Ware (Hirshabelle), Sharif Hassan Sheikh Aden (Jimbo la Kusini Magharibi) na Sheikh Ahmed Madobe wa Jubaland ambaye alikuwa mwenyeji wa mukutano huo. Hisia za maoni katika mikutano yote viongozi hao waliitisha kusitishwa kwa mahusiano kati ya serikali za majimbo na serikali kuu (Mogadishu) kwa kisingizio kuwa Rais Farmajo ameshindwa kupigana na Al Shabaab na muendelezo wake wa kuingilia mambo ya ndani ya serikali za majimbo. Sheikh Ahmed Madobe alikuwa gavana wa Kismayo kuanzia 2006 chini ya Muungano wa Mahakama za Kiislamu (ICU) kabla kuvunjwa na uvamizi wa Ethiopia iliyoegemea Marekani.

Serikali ya Kenya inayoegemea Uingereza iliingia

Endelea Uk..6

JARIDA LA
UQAB

Somalia kuhifadhi maslahi ya bwana wake. Hivyo basi, Jeshi la Ulinzi wa Kenya (KDF) mnamo 16 Oktoba 2011 kwa kisingizio cha "kupambana na ugaidi" iliivamia Somalia na kujumuika safu moja na Sheikh Ahmed Madobe ambaye alikuwa anaongoza Kundi la Ras Kamboni, ambalo ni kundi la kijeshi lilitotokana na Vuguvugu la Ras Kamboni. Kwa pamoja wakaikomboa Kismayo na hivi sasa iko chini ya Madobe kama rais wa Jimbo la Jubaland Somalia. Eneo la mzozo ambalo lina utajiri wa mafuta linapakana na Jimbo la Jubaland Somalia.

Serikali Kuu ya Somalia ambayo inaegemea Marekani ilipoona hatari inayotokamana na majimbo yanayoegemea Uingereza wakiongozwa na Sheikh Ahmed Madobe wakazindua kampeni pana ya kuwabdalisha viongozi wa majimbo. Hivyo basi, njama zao zikapelekea kubadilishwa kwa Sharif Hassan Sheikh Aden (Jimbo la Kusini Magharibi) akaingia Abdiaziz Hassan Mohamed, aliyekuwa katika serikali kuu kama waziri wa kawi na rasilimali za maji kwa kushinda kura mnamo Jumatano, 19 Disemba 2018. Abdiweli Mohamed Ali Gaas (Puntland) akaondoshwa na kuingia Said Abdullahi Deni, aliyekuwa katika serikali kuu kama waziri wa mipango kwa kushinda kura mnamo Jumanne, 8 Januari 2019. Matokeo ya uchaguzi wa majimbo yaliyobakia ya Hirshabelle, Jubaland na Galmadug hayajulikani lakini inaonesha wazi kuwa uongozi wa serikali za majimbo una wasiwasi kiasi kwamba mnamo Oktoba 2018 Mohamed Abdi Ware (Hirshabelle) alitangaza kuwa atashirikiana na serikali kuu (Mogadishu) na matokeo ya uchaguzi wa Agosti 2019 katika kinyang'anyiro cha Jubaland ambapo Sheikh Ahmed Madobe anaona aking'olewa mamlakani na serikali kuu!

Kutokana na sababu hizo ni wazi kuwa kelele za mzozo wa hivi majuzi kati ya Kenya na Somalia si chochote isipokuwa ni njama za kisiasa kati ya mataifa koloni yakijaribu kipingana kwa mujibu wa maamrishi ya mabwana zao wamaghari ambayo yanalenga kuhifadhi maslahi yao. Somalia ikaipa onyo Kenya kwa kuwa mwenyeji wa Kongamano la Mafuta ya Somalia mjini London mnamo 7 Februari 2019. Kenya kwa upande mwingine, ikajibu kwa hasira kutokana na tishio kubwa kwa maslahi ya bwana wake nchini Somalia na hususan Jimbo la Jubaland. Ikimaanisha kuwa kura zinazokuja Agosti 2019 ndani ya Jubaland ni tishio la moja kwa moja kwa Uingereza.

Kenya na Somalia zinatawaliwa na mfumo batili wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake zinazonuka ikijumuisha Demokrasia. Mfumo muovu unaojali tu uporaji wa rasilimali kupitia makampuni ya kimagharibi na kuwaacha watu katika hali za umasikini wa kupindukia! Zaidi ya hayo, Somalia ni ardhi ya Waislamu ambayo miji yake ya kisasa kama Mogadishu ilikuwa chini ya Khilafah ya Abdul Malik Marwan. Mnamo 1875, Waislamu waliteka Kismayo na ikawekwa chini ya

Khilafah Uthmaniyya ikitawaliwa na Sultan Abdul Aziz bin Mahmoud II na kuunganishwa katika Wilaya ya Misri chini ya Wali Ismail Pasha.

Suluhisho msingi na dharura kwa mzozo wa bahari ni kwa uongozi wa nchi mbili hizo na hususan Somalia kwa kuwa ni taifa la Waislamu kukata mahusiano yake ya kimataifa na kukumbatia mwito wa kurudisha tena maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume. Khilafah iliyosimamishwa kwa kutozingatia mipaka ya kikoloni ambayo inalenga kuleta husuma kati ya watu kwa kupia debe utaifa! Wakati huo huo rasilimali zinasambazwa kwa haki kati ya raia chini ya Khilafah ili kuhakikisha mahitaji msingi ya watu binafsi, mujtama na ya ziada ya watu binafsi yanakidhiwa kwa ukamilifu ndani ya uwezo wake. Ama kwa taifa la Kenya lisilokuwa la Waislamu ni lazima liurudie Uislamu kama mfumo, liusome na kuulinganisha pasi na kutia maanani tafsiri za kimagharibi juu ya Uislamu. Ni chini ya Khilafah pekee ndipo Kenya, Somalia, Afrika na ulimwengu kwa ujumla utakapopata utulivu, maendeleo na ustawi wa kweli kutokana na utekelezwaji kikamilifu wa Shari'ah (Qur'an na Sunnah) chini ya Khalifah muadilifu anayeongozwa na Uislamu PEKEE.

Ali Nassoro Ali
Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

Kujitoa Muhanga Nafsi yako, Fedha zako na Wakati wako, ni moja katika sifa muhimu za Mbebaji Da'wah

Kubeba Da'wah ni kazi kubwa mno na ni njia iliyojaa magumu na matatizo, njia ambayo ilipitiwa hapo awali na Mtume wetu (saw) na Maswahaba zake (ra) na kuikabidhi wale ambao wameiamini Da'wah hii baada yao; ili kumlingania mwanadamu kutoka katika kuabudu viumbe na kumuita katika kumuabudu Muumba pekee. Hakuna ambaye anaweza kuyabeba magumu na matatizo ya njia hii isipokuwa mtu ambaye amejifunga, amejirekebisha na kujikuza mwenyewe kwa sifa za uzuri ambazo ni lazima awe nazo mbebaji Da'wah na sifa kubwa katika hizo ni 'kujitoa muhanga.'

Kujitoa muhanga inamaanisha: kupeana kitu pasi na kutarajia chochote, mfano kujitoa muhanga nafsi yako, fedha zako, kazi yako, muda wako, familia yako, elimu yako, cheo chako n.k mpaka mtu anahisi kuwa ana haki tu ya mahitaji msingi na si chengine chochote, kwa hiyo wanafanya bidii katika kujitoa muhanga pasi na kutafuta malipo ya kimada kutokana na mchang'o wao lakini wanatafuta radhi za Mwenyezi Mungu (swt) na kuinurusu Dini Yake.

Hakika, kufaulu hakufikiwi kwa matumaini na ubebaji Da'wah (ulinganizi wa Uislamu) umejengwa juu ya kila aina ya juhudhi na kujitoa muhanga. Lau itafikia kuwa maradhi yametumwa juu ya wabebaji Da'wah ni jambo la kuendelea, basi itakuwa ni urongo kwa Da'wah ya haki kuweza kusimamishwa pasi na kujitoa muhanga.

Kujitoa muhanga kibinasi ni sifa ambayo inatakiwa kubebwa na mbebaji Da'wah na lazima apambane na yatakayomfika katika njia hii; ya mateso, kukataliwa, kushtakiwa, kukatwa kwa mapato, kufungwa na kudhibitiwa katika nyanja zote za maisha. Anaweza hata kuuliwa. Na hadithi za Mitume na Manabii na maswahaba zao, ikijumuisha Mtume Muhammad (saw) na maswahaba zake, waliweka mfano mzuri kwetu sisi.

Kipenzi chetu Mtume (saw) hakuwa salama katika njia hii ya kuufikisha Uislamu kutokana na madhara ya wasioamini. Tokea alipopanda Mlima Safa na kuonya kabilia lake waliokuwa karibu, alianza kupata madhara ya kila aina, walimzushia kuwa ni mchawi na mwenda wazimu baada ya kujulikana kuwa ni mkweli na muaminifu. Yeye (saw) na maswahaba zake walipata madhara makubwa na walifika na mitihani mizito. Hivyo basi, Mtume (saw) alianza kujiwasilisha kwa makabila wakati wa msimu wa Hajj akiomba nusrat (ulinzi) ili aweze kulingania Dini ya Mwenyezi Mungu. Alikwenda Ta'if akitafuta lengo lake lakini alirudi huku miguu yake imejaa damu na kufurushwa, na alitengwa yeye, maswahaba zake na waliomuunga mkono katika majangwa ya Makkah kwa miaka 3 kiasi kwamba walikula majani ya miti kutokana na njaa.

Maswahaba wengi wa Mtume (saw) walionyesha

juhudhi na kujitoa muhanga kwa hali ya juu; Bilal, Sumayyah, Yasser na Ammar waliteswa vibaya mno kiasi kwamba Sumayyah (ra) na Yasser (ra) waliuliwa katika njia ya 'Aqeedah' walioshikamana nayo katika maisha, wakitafuta malipo ya Mwenyezi Mungu na pepo ambayo upana wake ni kama mbingu na ardhi. Maqruraysh pia walimpiga Abdullah bin Mas'oud (ra) vibaya mno mpaka damu ikamjaa usoni mwake kwa kuwasomea aya alizoteremshiwa Mtume (saw). Alifurahi na kupata nishati kutokana na yale yaliyomfika, akijua fika kuwa aliyokumbana nayo yatahifadhiwa na Mwenyezi Mungu (swt); na ndiyo akasema "Wale maadui wa Mwenyezi Mungu hawajawahi kuwa duni thamani kwangu kuliko wakati huu, na lau mtataka nirudi tena kwao na nikawafanyie tena kesho." Wakasema, 'La, inatosha kwako wewe. Umewafanya kusikiza ambacho wanakichukia.' Mus'ab (ra) anatoka na kuacha nyuma starehe na kuhamia Madina kama mlinganizi wa Uislamu; Ali (ra) anajiweka katika hatari ya kuuliwa katika kitanda cha Mtume (saw) usiku wa Hijrah; Al-Baraa' alijitupa katika Bustani la Kifo kati ya maadui; kisha, Mwenyezi Mungu (swt) anawapa ushindi Waislamu kwa sababu yake, Abu Dardaa' aliwachana na biashara na kujifunga na ukuruba wa Mtume (saw); Khalid bin al-Waleed alikubali kuacha na cheo chake kwa kumuheshimu Ameer wa Waumini; Abu 'Ubaydah aliwacha cheo chake cha mkuu wa jeshi na kumpa Amr bin Al-Aas ili aweze kuwaunganisha Waislamu.

Da'wah yoyote ile husambazwa kwa juhudhi za wafuasi wake, na Dini ya Uislamu haikusambaa kupitia utulivu wa miyo na usalama wa nafsi. Dini ya Uislamu isingetufika pasi na juhudhi kubwa ya maswahaba wa Mtume (saw) na Waislamu waliokuja baada yao ambao waliacha nyumba zao, familia zao, watoto na biashara zao na kujitoa muhanga nafsi na mali zao kwa ajili ya hilo. Walifahamu kuwa wanabebea jukumu zito na adhimu kwa kuwa wao ni warithi wa Mtume (saw) katika ulinganizi wa Mwenyezi Mungu na utekelezaji wa hukumu za Mwenyezi Mungu ndani ya Dola ya Khilafah ili watu wawezee kupata haki na huruma ya Uislamu na kuingia katika dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi. Hivyo basi, chochote kando na hili jukumu adhimu na kubwa ilikuwa ni jambo duni machoni mwao.

Ama kuhusu kuzitoa muhanga fedha zao, maswahaba wema ndio kiigizo chema kwa wabebaji Da'wah katika utoaji na ukarimu kuhusiana na mali zao. Ulinganizi wahitajia fedha na michango ili kuweza kutekeleza kazi zake na nani mbora au anyestahiki zaidi kuliko mbebaji Da'wah katika kuigharamikia Da'wah hii na kazi zake, kujifunga kuigharamikia kifedha kama anavyojifunga kwa watoto wake na walioko chini ya usimamizi wake na huwa mbioni kufanya khair ili kuitikia maneno ya Mwenyezi Mungu (swt):

وَمَا شَفَقُوا مِنْ شَيْءٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يُوفِي إِلَيْهِمْ وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ

"Na mkitoa chochote katika Njia ya Mwenyezi Mungu mtarudishiwa, na wala nyinyi hamtadhulumiwa." [Al-Anfal: 60]

إِنَّ الَّذِينَ يَتَّقُونَ كُلُّهُمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًا وَعَلَانِيَةً
يَرْجُونَ تِجْرِيَةً لَنْ تَتَّوَرَ * لِيُوَفِّيهِمْ أَجُورُهُمْ وَيَرِيدُهُمْ مِنْ فَضْلِهِ إِنَّهُ عَفُورٌ شَكُورٌ

"Hakika wale wanao soma Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na wakashika Sala, na wakatoa kwa siri na kwa dhahiri katika tulivyowaruzuku, hao hutaraji biashara isiyo bwaga. Ili Yeye awalipe ujira wao kwa ukamilifu, na awazidishie kutokana na fadhiba zake. Hakika yeye ni Mwenye kusamehe Mwenye shukrani." [Faatir: 29-30]

الَّذِينَ يَنْفَقُونَ أَمْوَالَهُمْ بِالْيَمِينِ وَالْيَمِينَ فَلَهُمْ أَجْرٌ هُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا
خُوفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزُنُونَ

"Wale wanao toa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi; wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika." [Al-Baqara: 274]

مَثُلُ الَّذِينَ يَنْفَقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمَثُلُ حَبَّةٍ أَنْبَتَتْ سَبَعَ سَنَابِلَ فِي كُلِّ
سَبْلَةٍ مَائِةٌ حَبَّةٌ وَاللَّهُ يَضْعِفُ لِمَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ وَسِعٌ عَلِيمٌ

"Mfano wa wanao tumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje iliyo chipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Na kwa Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mwenye kujua." [Al-Baqara: 261]

Ziko aya nyingi katika Qur'an ambazo zinakokoteza kugharamia njia ya Mwenyezi Mungu. Zifuatazo ni Hadith za Mtume (saw) ambazo zinatilia shime kugharamika kwa njia ya Mwenyezi Mungu:

ما من يوم يصبح العبد فيه إلا مكان ينزلان، يقول أحدهما: اللهم اعطِ منفأً
خلفاً، ويقول الآخر: اللهم اعطِ ممسكاً تلها

'Kila siku malaika wawili hushuka chini kutoka Mbinguni na mmoja wao husema: 'Ewe Mwenyezi Mungu! Mlipa kila mtu anayetoa katika njia Yako,' na malaika mwiningine husema: 'Ewe Mwenyezi Mungu! Muangamize kila bahili'." (Bukhari: Na. 1374)

وعن أبي هريرة رضي الله عنه أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال: «قال
الله: أتفق يا ابن آدم أتفق عليك» رواه البخاري ومسلم

Abu Hurairah amesimulia kwamba Mtume (saw) alisema: "Mwenyezi Mungu amesema, 'Tumia (katika sadaqa) Ewe mwanadamu, na Mimi nitatumia juu yako" [Sahih Al-Bukhari na Muslim]

Maswahaba (ra), walifahamu maana yake kwa usahihi na kuzifanya kazi, wakiyelea mifano yao kuwa ndiyo misingi na mwangaza unao muongoza yeyote anayefuata njia yao. Abu Bakr Al-Siddiq (ra), aliyeana mali yake yote kwa Mtume (saw) kwa sababu hiyo Mtume (saw) akamuuliza: "Umeiwachia nini familia yako?" Akajibu kuwa: "Nimewaachia Mwenyezi Mungu na Mtume (saw)." Uthman bin Affan (ra) akaligharamikia jeshi la al-Usra mpaka Mtume (saw) ما ضر عثمان ما فعل بعد «اليوم» "Hakuna kitakacho mdhuru Uthman baada ya aliyyafanya leo", na kukinunua kisima ndani ya Madinah kutoka kwa Myehudi mwanamume na kukitoa kama zawadi kwa wakaazi wa Madinah. Abu Talha aliitoo

sadaqa mali yake iliyokuwa kipenzi Beeruha (busani) kwa Mtume (saw) na kumwambia aitumie apendavyo baada ya kusikia aya ya Mweynezi Mungu (swt): لَنْ تَنَالُوا الْبَرَ حَتَّىٰ شَتَّقُوا مِمَّا ثَجُونَ وَمَا شَتَّقُوا مِنْ شَيْءٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ

"KABISA HAMTAFKIA wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda. Na kitu chochote mnacho kitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua." [Aal-Imran: 92]

Suhayb alipoteza mali yake yote kwa ajili ya kumfuata Mtume (saw) kwenda Madinah. Maswahaba wa Mtume (saw) walikuwa wakishindana katika juhud, ukarimu na kugharamia katika njia ya Mwenyezi Mungu, japo kwa kidogo, walikuwa na ari ya kutekeleza khair hii kwa kuwa walijua na walikuwa na yakini kuwa kila wanacho gharamikia kitahifadhi kwao na Mwenyezi Mungu (swt). Nguvu zao katika kuitumikia njia hii ya khair ili wafanya masikini mionganoni mwa Maswahaba kumshitakia Mtume (saw) kwamba hawana chochote cha kutoa (sadaqa) na kwamba watu matajiri wanawashinda katika malipo. Muslim ameripoti kutoka kwa Abu Hurayrah (ra) aliyesimulia:

أن فقراء المهاجرين أتوا رسول الله صلى الله عليه وسلم فقالوا: ذهب أهل
الدثور بالدرجات على والنعيم المقيم، فقال: وما ذاك؟ قالوا يصلون كما نصل،
ويصومون كما نصوم، ويتصدقون ولا نتصدق، ويغتنمون ولا نغتنم، فقال رسول
الله صلى الله عليه وسلم أفالآنكم شيئاً ترکون به من سبقكم وتسبقون به من
بعدكم؟ ولا يكون أحد أفضل منكم إلا من صنع مثل ما صنعتم، قالوا: بل يـا
رسول الله، قال: تسبحون وتكبرون وتحمدون رب كل صلاة ثلاثة وثلاثين مرـة

"Masikini mionganoni mwa Muhajirun walikuwa kwa Mtume (saw) na kusema: Watu matajiri wana malipo yote; wanasali kama tunavyosali, wanafunga kama tunavyofunga na wana mali ya ziada ambayo wanatoa katika sadaqa; lakini sisi hatuna mali ambayo twaweza kutoa katika sadaqa." Mtume (saw) akawaambia: "Je nisiwafunze matamshi ambayo yatawafanya mufikie daraja ya wale wanaowashinda? Hakuna atakayefikia daraja yenu isipokuwa yule anayefanya kama nyinyi." Wakasema: "Kwa nini usitufunze, Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: "Mpwekesheni Mwenyezi Mungu (semeni: Mwenyezi Mungu ni Mkubwa) baada ya kila sala mara thelathini na tatu; na kumsifu Mwenyezi Mungu (semeni: Sifa Njema ni za Mwenyezi Mungu) baada ya kila sala mara thelathini na tatu; na kumtukuza (semeni: Utukufu ni kwa Mwenyezi Mungu) baada ya kila sala mara thelathini na tatu."

Mbebaji Da'wah anazoea kutoa sadaqa hata kama ni kidogo, wakati wa umasikini na uhitaji hususan wakati wa majanga na uadui ambao mahitaji ya Da'wah huzidi na huhitaji kujitoa muhanga zaidi, ataipa hadhi nafsi yake kwa kuisafisha kutokana na kuipenda Dunia. Mlango wa kuigharamikia Da'wah ambayo itarudisha tena utukufu kwa Waislamu na kurudisha tena ubwana wao katika haya maisha kwa mara nydingine tena ni moja ya milango bora ya khair na inajumuisha khair zote kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu.

Ama kuutoa wakati muhanga, kama ilivyo muhimu kwa mbebaji Da'wah kutenga wakati wake kwa Da'wah usiku na mchana, na kutenga wakati wake bora ili

Endelea Uk..9

kutekeleza amana aliyochagua kuibeba, kwa kuiamini kuwa ndiyo njia ya mwamko wa Ummah kutokana na madhara ya maisha haya mafupi, na kujitenga kwake na Mwenyezi Mungu na kutawaliwa na maadui. Mbebaji Da'wah huutoa muhanga wakati wake bora kwa ajili ya Da'wah hii na kufanya kuwa ndiyo kipaombele katika maisha yake akitafuta radhi za Mwenyezi Mungu (swt) kama malipo, akiyatoa muhanga mapumziko yake na kulala kwake na hata kutoa muhanga wakati wa ajira yake kwa ajili ya Da'wah ya Mwenyezi Mungu, akiyatoa kuwa Mwenyezi Mungu (swt) anamuhifadhi muhanga wake kwa Siku ambayo hakuna pesa wala watoto watakaomnifaisha mtu na kwamba ataubariki wakati wake na vitendo vyake na rizq yake. Akiwa na yakini kwamba rizq yake itamfikia na haitopungua mfano wa punje –ima atafanya kazi kwa saa 20 au 8, au zaidi au chini kwa sababu rizq yake ishaandikwa na hatokufa kabla kuimiliki yote.

Ni imani hii inayomsukuma mbebaji Da'wah katika ulinganizi wa da'wah yake muda wote popote alipo: ajirani, nyumbani na familia yake, watoto wake na majirani, mjini mwake, anazungumza ukweli, anaamrisha mema na kukataza maovu, akigawanya muda wake kati ya ajira yake, masomo jumla na maalumu, akitembelea walengwa na kufanya kila ambalo Da'wah yamuhitajia kufanya. Daima yuko tayari kufanya lolote atakalo agizwa pasi na kusitasita au kucheleva. Ni mchangamfu na mcheshi, mwenye moyo wa huruma kwa watu, mwenye kuwapenda khair, kujali manufaa na maslahi yao, yuko makini kuhakikisha ana wahamisha kutoka katika hali ya kumchukiza Mwenyezi Mungu (swt) hadi katika hali ya kumfurahisha Mwenyezi Mungu (swt). Anawapenda yale anayoipendea nafsi yake na kuwafikishia kile alichoruzukiwa na Mwenyezi Mungu katika ruwaza safi kiufahamu na kwa uwazi.

Hizi saa na dakika ambazo twaishi katika dunia ndiyo umri wetu; lazima tuzijaze ndani yake twaa na radhi za Mwenyezi Mungu (swt), tusipoteze katika starehe, hata kama imeruhusiwa na kuacha yale ambayo Mwenyezi Mungu ametuamrisha juu yetu. Kila binadamu lazima ajiwekee mpangilio maalumu wa siku wa kazi yake (hususan mbebeji Da'wah) ili kujihesabu katika mapungufu yake kabla hajahesabiwa. Kurekebisha mapungufu aina yoyote katika haya maisha inawezekana, lakini Akhera hakuna kazi isipokuwa majuto na majonzi kutokana na uhalifu na hakika majuto yatakuwa hayasaidii.

فَعَنْ أَبِي بَرْزَةَ نَضْلَةَ بْنِ عَبْدِ الْأَسْلَمِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: «لَا تَزُولُ قَدْمًا عَبْدٌ يَوْمَ الْقِيَامَةِ حَتَّى يَسْأَلَ عَنْ أَرْبَعَةِ فِيمَ أَفَاهَ؟ وَعَنْ عِلْمِهِ فِيمَ قَعَلَ؟ وَعَنْ مَا لَهُ مِنْ أَيْنِ اكْتَسَبَهُ؟ وَفِيمَ أَنْفَقَهُ؟ وَعَنْ جَسْمِهِ فِيمَ أَبْلَاهُ» رواه الترمذى.

Abu Barza al-Aslami (ra) ameripoti kuwa Mtume (saw) alisema, "Miguu miwili ya mwanadamu haitoacha (kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu) Siku ya Hukumu mpaka atakapoulizwa kuhusu mambo manne: kuhusu umri wake na alivyoitumia, elimu yake na alivyoitumia,

mali yake na alivyoichuma na alivyoitumia; na mwili wake namna alivyoitumia. [Sahih, ameripotiwa na At-Tirmidhi] وَعَنْ أَبْنَ عَبَّاسِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لِرَجُلٍ وَهُوَ يَعْظِمُهُ: «أَغْتَمْتُ خَمْسًا قَبْلَ خَمْسٍ: شَبَابَكَ قَبْلَ هَرْمَكَ، وَصَحْثَكَ قَبْلَ سَقْمَكَ، وَغَنَاعَكَ قَبْلَ فَقْرَكَ، وَفَرَاغَكَ قَبْلَ شَغْلَكَ، وَحَيَاتَكَ قَبْلَ مَوْتَكَ» رواه الحاكم
[المستدرك]

Ibn Abbas ameripoti kuwa Mtume (saw) alisema, "Patiliza mambo matano kabla matano: ujana wako kabla uzee wako, afya yako kabla maradhi yako, utajiri wako kabla umasikini wako, muda wako uliokuwa na nafasi nao kabla kazi zako, uhai wako kabla mauti yako." [Imesimuliwa na Al-Hakim katika al-Mustadrak]

Ni wazi na inaonekana kuwa Mwenyezi Mungu (swt) alibariki zama za wanavyuoni wa kweli, waliweza kufanya mambo makubwa pasi na kuyadhania kimahesabu ya kimada, naye Mwenyezi Mungu (swt) akayabariki maneno, vitendo na vitabu vyao na wakafikia upeo wa kunufaisha na kuathiri ambaa haikuwahi kutokea kwao na wameutoa muda wao muhanga mkubwa. Natija ya muhanga katika hali na juhuza zote ni malipo, manufaa na muongozo asiodiri mtu isipokuwa Mwenyezi Mungu (swt) ndiye anayejua kama alivyosema Mtume (saw):

من دعا إلى هدى كان له من الأجر مثل أجور من تبعه، لا ينقص ذلك من أجورهم شيئاً

"Yeyote anayelingania katika uongofu atakuwa na malipo sawa na wale wanaomfuata, bila kupunguziwa chochote katika malipo yao."

وَعَنْ أَبِي مَسْعُودَ الْأَنْصَارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: مَنْ دَلَّ عَلَى خَيْرٍ فَلَهُ مِثْلُ أَجْرِ فَاعِلِهِ

Abu Mas'ud Al-Ansari (ra) ameripoti: "Yeyote anayemuongoza mtu katika khair atalipwa malipo sawa na yule anayetekelez kitendo hicho cha khair."

وقال رسول الله صلى الله عليه وسلم لعلي رضي الله عنه يوم فتح خير في حدث طويل: فوالله، لأن يهدى الله به رجلًا واحدًا خير لك من أن يكون لك حمر النوع

Mtume (saw) alimwambia Ali (ra) siku ya kuifungua Khaybar: "Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, lau mtu mmoja ataongozwa na Mwenyezi Mungu kuititia wewe, itakuwa bora kwako kuliko zaidi ya ngamia wekundu." Mwisho kabisa, kwa kuwa Da'wah imekitwa katika kujitoa muhanga, basi kila mbebaji Da'wah anafahamu nini la kufanya.

Ewe Mwenyezi Mungu, tunakuomba utupe utambuzi wa yale yaliyo ya sawa, khair, mbinu zilizo bora katika mazungumzo na vitendo na tufanye sisi tuwe ni wenye kusikiza kwa makini yale yote yanayosema na kufuata yale yaliyo bora na tufanye sisi kuwa ni funguo za khair na kufuli za maovu na tupe zawadi ya Fadhila Zako, Khair na Ukarimu wa Khilafah kwa njia ya Mtume, Ewe Bwana Mwenye Nguvu na Utukufu. Maombi yetu ya mwisho ni Alhamdulillahi Rabbil 'Aalamin, Amani na Baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad, familia yake na maswahaba zake.

Chanzo: Jarida la Al-Waie, Toleo 387, Rabi'ul Akhir 1440 H – Disemba 2018 M

Sababu za Kuvunjika kwa Familia Miongoni mwa Jamii za Waislamu walioko Magharibi

Ndoa ni moja katika mahusiano muhimu tutakayojifunga nayo maishani mwetu. Ni fungamano linaloathiri na lililokitwa chini ya mafungamano mengine muhimu, kwa mfano mafungamano tutakayokuwa nayo na watoto na wajukuu wetu. Uislamu unatufunza kuwa ndoa ni taasisi ya kisheria ambayo mwanamume na mwanamke wanaweza kuingia katika mahusiano ya ukaribu. Tunapojifunga na mahusiano aina hiyo tunamatumaini ya kujenga mahusiano ya utulivu kwa msingi wa uswahiba amba si tu kwa ujenzi wa mazingira ya uchajimungu ya malezi ya watoto bali pia ni njia ya kuimarisha mahusiano na Muumba wetu (swt).

«إِذَا تَرَوْجَ الْعَبْدُ فَقَدِ اسْتَمْلَ نِصْفَ الدِّينِ فَلَيْقَ اللَّهُ فِي النِّصْفِ الْبَاقِي»

“Mtume Muhammad (saw) ametuambia kuwa mtu anapooa, amekamilisha nusu ya dini na hivyo anatakiwa kumcha Mwenyezi Mungu kuhusiana na nusu iliyobakia.” [Al-Tirmidhi Hadith 3096 imesimuliwa na Anas ibn Malik]

Lakusikitisha, uhalsia uliopo leo Magharibi ni kuwa ndoa nydingi ndani ya jamii ya Waislamu zinavunjika na kuishilia katika talaka, na ndoa ambazo bado zimehimili ziko mbali na matumaini tuliyoyataja hapo juu. Utafiti wa mwaka 2000, uliofanyika ndani ya jamii ya Waislamu ndani ya Marekani, uliweka talaka kuwa asilimia 30. Utafiti mpya unaonyesha kuwa asilimia hii inazidi kukuwa na kwamba matatizo yanayohusiana na kuvunjika kwa maisha ya ndoa yanazidi ndani ya jamii ya Waislamu wanaishi Magharibi.

Kwa sababu hii, ni muhimu kwamba tunafahamu hatari iliyopo ndani ya mujtama za uhuru (kiliberali) za kimagharibi hususan zinazopelekea talaka. Hivyo basi, tutweza kujilinda kwa kadri ya uwezo wetu dhidi ya vigezo hivi na kutumaini kupunguza idadi ya ndoa zinazovunjika ndani ya jamii ya Waislamu.

Ufahamu juu ya ndoa unatofautiana pakubwa tunapoliganisha mtizamo wa kiliberali wa kimagharibi na ule wa Kiislamu. Ndani ya Magharibi ndoa ni kitu cha khiyari kuhusiana na mwanamume na mwanamke kuingia katika mahusiano baina yao kwa kuwa uhuru (uliberali) hauzingatii maadili katika ukaribu. Unamuachia mtu binafsi kujiamulia ima kuingia katika ndoa kabla kuingia katika mahusiano au kuwa na mahusiano kabla ya ndoa, mfano ngono ya usiku mmoja au hata mahusiano ya ndani ya ndoa. Hili limefungua milango ya kila aina ya mahusiano yanayoifanya taasisi ya ndoa kuwa dhaifu na kuchukiwa kiukweli. Hii fikra ya kufuata matamanio na kufanya unavyotaka ili kujifurahisha pia inaathiri jamii ya Waislamu. Kwa hivyo tunaona matatizo kila aina kwa nini na lini Waislamu kiukweli wanaingia katika ndoa (mfano msukumo kutoka kwa familia na jamii baada ya kuwa na mahusiano ya nje ya ndoa

ya muda mrefu au baada ya mtu kuona kuwa maisha yake yamekuwa “sawa”). Sababu hizi kiasili hazitokani na Uislamu na zinaweza pia kuathiri kufaulu kwa ndoa hususan pale ambapo wanandoa wana sababu tofauti za kuoana.

Wakati ufahamu wa ndoa unapoingia maradhi ya fahamu zisizokuwa za Uislamu, kikawaida hili hupelekea matatizo mengi. Kwa mfano, ndoa ndani ya Magharbi zimekuwa biashara ambazo kuptitia kwake kiwanda kikubwa Kimechipuza. Kupeana kipaombele juu ya “siku kubwa” hilo pekee limekuwa na athari juu ya jamii ya Waislamu. Pale ambapo eneo la ufanyaji harusi limejaa israfu ya chakula, mavazi ya maharusi, mapambo ya dhahabu na magari ya ghali yanakuwa “jambo la lazima” katika siku hiyo kubwa, wachumba wachanga wengi wanalazimika kuisimamisha harusi yao au kuchukua mikopo ya haramu. Hatima yake ni kuifanya siku ya ndoa kuwa kikwazo katika kushikamana na hukumu za Uislamu. Ziada ni kuwa watu wana lazimisha mahari kubwa na kuwa uzito zaidi kwa wachumba wachanga kuanza maisha ya ndoa. Wakishinikiza zaidi siku ya harusi yenye na kuyapa Kipaombele mambo ya kimada na kuyasahau maneno ya Mtume (saw) aliposema kuwa:

«أَعْظَمُ النِّسَاءِ بِرَكَةً أَيْسِرِهِنْ صَدَاقَةً»

“Mmoja (kati yenu wanawake) anayepokea kiwango cha chini cha mahari ndiye mwenye baraka zaidi. [Imepokewa na al-Haakim kutoka kwa Aisha]

Lakusikitisha ni kuwa wachumba wachanga ndani ya Magharibi wanaanza maisha yao ya ndoa wakiwa na madeni makubwa yakiidhuru ndoa yao kwa matatizo ya kifedha kabla hata hayajaanza. Mbegu za kupenda mali (ulafi) huendelezwa katika ndoa pale ambapo wanandoa Waislamu wanapotaka kuwa kama kina “Joneses” au kina “Ahmed.” Kulelewa katika mujtama za kimagharibi pia tunajikuta katika ushindani wa matumizi (upapajia) kiasi kwamba mambo yasiyo lazima yanaharibu maisha ya familia kutokana na kuyaendea mbio mahitaji yasiyomuhimu na kuishi kwa mujibu wa kiwango cha maisha kilichowekwa na wengine!

Zaidi ya hayo, wanandoa hawashauriwi kwa mtizamo wa Kiislamu juu ya ndoa, mitizamo inayohusiana na maadili ya kiliberali ya kimagharibi hupenyezwa katika akili za wanandoa hawa. Mfano, tunaona namna wanawake wanavyowasilishwa kama zana za ngono katika mujtama za kimagharibi zinavyoathiri ndoa kwa ubaya. Wanawake wanawasilishwa kama vyombo vya matamanio na mapicha ya ngono yakisambazwa kuptitia biashara ya kujifurahisha na kiwanda cha video za ngono, si tu kwamba tunajenga mujtama ya ngono bali pia tunabuni matarajio ya kirongo kuhusu mahusiano

Endelea Uk..11

kati ya mwanamume na mwanamke yanavyotakiwa kuwa na ni yupi mwanamke mrembo na mwanamume anayestahili. Wote wanaume na wanawake wanaathiriwa na picha na mawazo haya, kiasi kwamba kuwapelekea kutafuta matarajio haya ya kirongo ndani ya nyumba zao na kuwaondosha humo ikiwa hawafikii viwango hivyo vya kipuzi. Ziada ni kuwa utafiti uliowasilishwa na Muungano wa Amerika wa Masuala ya Kijamii wa mwaka 2016 uliashiria kuwa idadi ya talaka huzidi pale wanandoa wanapoanza kuangalia video za ngono. Kudumu katika ngono na kutizama video za ngono ni tatizo la kweli ndani ya mujtama za Magharibi kama madawa na pombe, tatizo hili kwa masikitiko limeingia kisirisiri ndani ya jamii ya Waislamu pia na kuwafanya wanandoa Waislamu kuwa dhaifu na kupelekea talaka. Kwa kusikitisha, kuna ongezeko la mahusiano kabla ya ndoa katika jamii ya Waislamu na kuzidi kwa talaka kutokana na mahusiano zaidi ya ndoa.

Kuna mkanganyiko juu ya majukumu na haki za mume na mke kutokana na fikra zinazohusiana na thaqafa tofauti wanazoishi ndani yake – Thaqafa ya kimagharibi ambayo vijana wengi wanavutiwa na thaqafa ya Mashariki (inayoonekana kuwa ya Kiislamu) ambayo wazee wetu wengi wanaathiriwa nayo. Waislamu mara nyingi wana mchanganyiko wa mawazo yanayoathiriwa na thaqafa zisizokuwa za Kiislamu. Mchanganyiko huu wa fikra ndiyo pia chanzo cha mgogoro kati ya wanandoa. Kwa mfano ikiwa mmoja kati ya wanandoa amebeba mtizamo wa kimagharibi ambao uhuru na usawa wa kijinsia wa wanawake unapigiwa debe, inakuwa tatizo kwa mwanandoa mwengine ambaye amebeba mtizamo wa kimashariki unaomuangalia mwanamke kama mtumwa kwa mumewe ambaye jukumu lake ni kutumikia mahitaji ya mumewe. Kiuhalisia, tunaona mchanganyiko wa fikra ambapo dori ya mchumaji mkate na msimamizi wa nyumba inakabidhiwa wanawake. Kwa hiyo anajipata akibeba mzigo wa kifehda kuisimamia familia na kuendelea kubeba majukumu ya Kinyumbani. Hili limepelekea kuvunja thamani ya umama, jukumu adhimu la mwanamke katika Uislamu. Ni muhimu tujifunze kuwa kuna chaguo la tatu: Uislamu –ambao umeweka wazi majukumu na haki za wanandoa wote ndani ya ndoa. Mwanamume ndiye kiongozi wa nyumba na hivyo ana majukumu ya kuisimamia kifedha ili kukimu mahitaiji ya familia yake. Ilhali majukumu ya mke ni kuwa msimamizi wa nyumba na mlezi wa watoto wake. Anaweza kufanya kazi nje ya nyumba lakini haitakiwi kamwe kuliona suala hilo kuwa la lazima. Uwazi katika haki na majukumu ya wote wanaume na wanawake kwa mujibu wa Uislamu ndiyo msingi wa utulivu ndani ya ndoa.

Pamoja na hayo ni kuwa wanandoa Waislamu wanapokumbana na matatizo yao ndani ya ndoa, tunaona kuwa talaka imekuwa jambo la rahisi kama chaguo katika kusuluhisha matatizo yao kama inavyoshuhudiwa katika mujtama jumla ndani ya Magharibi. Katika mujtama za kliberali, mtizamo ni

kuwa ndoa hazitakiwi kudumu kimsingi bali zilitakiwa kuboresha furaha yetu na punde hili linapokosekana, kwa nini tuendelee na mahusiano hayo? Huu ndio mtizamo wa kufikiria unaotokamana na mtizamo wa kliberali wa kimagharibi juu ya maisha ambapo furaha ya mtu binafsi ndiyo kipaombele kinyume na ahadi na uaminifu.

Mwisho, ni lazima tuisahau kwamba katika Uislamu mke sio mshirika wa mumewe; bali ni mwandani wake. Kuishi kwao pamoja hakukujengwa kwa mujibu wa ushirika bali kwa uswahiba na hukamilika na kuwa kitu kimoja katika nyanja ya maisha. Us wahiba ni pale ambapo kila mmoja anapata utulivu kutoka kwa mwensiwe. Mwenyezi Mungu ameifanya ndoa kuwa ndiyo chimbuko la utulivu kwa wanandoa wote.

(هُوَ الَّذِي خَلَقَهُ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجًا لِيُسْكُنَ إِلَيْهَا)

“Yeye ndiye aliye kuumbeni kutoka katika nafsi moja; na katika hiyo hiyo akamfanya mwensiwe wake, ili akae naye kwa utulivu.” [Al-A’raf: 189]

Yasmin Malik
Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

Halaqa 21: Usimamizi wa Mtume (saw) wa Shari'ah, Baada ya Kusimamisha Dola



Katika halaqa hii tutazungumzia usimamizi wa Mtume (saw) wa sheria, baada ya kusimamisha serikali.

Mtume (saw) siku ya kwanza, kufika Madina, alikuwa tayari ni msimamizi na mtawala mwenye mapenzi ya kupeleka mambo ya raia wake kwa mujibu wa nidhamu ya Mwenyezi Mungu (swt).

Miongoni mwa mambo aliyo yatekeleza Mtume (saw) kivitendo na yaliyo ashiria wazi wazi kwamba kweli alikuwa mtawala wa Dola na msimamizi kamili wa mambo ya raia ni: -

- Ujenzi wa misikiti
- Kujenga udugu kati ya Muhajirina na Answar
- Kufunga mikataba na Mayahudi
- Kuweka katiba ya watu wa Madina
- Usimamizi wa nidhamu ya uchumi na kijamii.
- Kutuma Saraaya/vikundi huku na kule; ili kubeba risala ya Uislamu kwa ulimwengu.

Kisha Aya za upangiliaji sheria zikaanza kuteremka na kutatua kila jambo, na kuhukumu kila kitu.

SWALI/JAWABU:

Ukweli wa Kura ya Maoni ya Mradi wa Kujitoa kwa Uingereza (Katika Muungano wa Ulaya)!



Swali

Bunge la Uingereza mnamo 16/1/2019 liliupigia kura mswada wa kutokuwa na imani na serikali ya May, lakini ye ye akashinda: (Waziri Mkuu wa Uingereza Theresa May aliponea kushindwa mnamo Jumatano katika bunge la House of Commons kufuatia mswada wa kutokuwa na imani na serikali yake uliowasilishwa na chama cha upinzani cha Labour. Alishinda imani kwa wingi wa kura 325 dhidi ya 306 ... matokea ya kura hizo ya mnamo Jumatano yanaonyesha kuwa takriban wanachama 100 wa Chama cha Conservatives waliopiga kura dhidi ya makubaliano mnamo Jumanne ya kujitoa huko kwa Uingereza, mnamo Jumatano walirudi na kupiga kura dhidi ya kutokuwa na imani na serikali ... AFP 16/1/2019) Je, hili tunalifahamu vipi? Takriban wanachama 100 wa Chama cha May walipiga kura dhidi ya mradi wake huo wa kujitoa huku wakiuruhusu upinzani kushinda, ikipelekeea kufeli kwa mradi huo wa May kwa kura 432 dhidi ya 202. Kisha Wabunge hao 100 walirudi na kupiga kura dhidi ya wapizani wa May, wakimruhusu May kushinda. Kana kwamba ni ugawanyaji dori! Na ni upi ufanuzi wa uidhinishaji wa mwanzo wa kujitoa kwa Uingereza mnamo 2016, lakini sasa kabla ya kutekelezwa kwake kwa takriban miezi miwili, unakataliwa?! Allah awajaze kheri.

Jibu

Uingereza ni mahiri katika uovu na ujanja, na katika kupanga na kuakhirisha ili kufikia malengo yake. Ili kupata jibu, tunatathmini mambo yafuatayo:

Kwanza, tutataja baadhi ya yale tuliyoyataja katika makala yetu ya mnamo 5/7/2016 baada ya kura ya maoni ya 23/6/2016, yaani, takriban miaka miwili na nusu iliyopita, tulipotarajia yale yaliyotokea katika kura ya sasa ya maamuzi ya Uingereza 15/1/2019:

1- Kura ya maoni ilifanywa nchini Uingereza mnamo 23/6/2016 ya kubakia au kuondoka katika Muungano wa Ulaya. Matokeo yalikuwa takriban asilimia 52 kuondoka, ambapo hatimaye Waziri Mkuu Cameron alitangaza kuijuzulu kwake na kwamba serikali hiyo itabakia kwa miezi mitatu. Katika kampeni yake ya uchaguzi, Cameron aliahidi kuwa atafanya kura ya maamuzi kwa mujibu wa tabia ya Uingereza ya kuweka ishara za kura ya maoni ili kufikia manufaa maalumu, kuititia kuutishia Muungano wa Ulaya na dola nyenginezo wanachama kwa ghasia za kisiasa na kiuchumi za azimio la kura hiyo ya maamuzi, endapo Uingereza itatoka katika Muungano huo.

2- Sera ya Uingereza ya kutumia kura ya maoni kama kitisho ili kupata maslahi kutoka kwa EU si

jambo jipya bali imelifanya jambo hili tangu miaka ya mwanzo ya kuingia kwa Uingereza katika muundo wa Ulaya. Uingereza imekuwa mwanachama wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Ulaya (EEC) tangu Januari 1973. Inaihifadhi sarafu ya "Pauni ya Sterling" na imesalia nje ya eneo la Schengen linalo wakilisha alama mbili kuu za hali maalumu ambayo Uingereza iliifurahia licha ya uanachama wake kwa EU. Imetumia fikra ya "kura ya maoni" kuhusu kubakia katika EU kama njia ya kuzitishia dola za Ulaya ili kupata maslahi zaidi kwa Uingereza ndani ya EU. Mnamo 1975 ilifanya kura ya maamuzi ili kuboresha hali za kubakia kwake ndani ya Muungano huo ambaao Waingereza walipiga kura wakipendelea kubakia ndani ya EEC, na hivyo kura za maoni za Uingereza ili kupata malengo ya sera hiyo zikafuata kwa hali kama hizo, hata kama ni kwa malengo maovu! Chama cha Tory kilisonga mbele kijanja katika kura ya maoni ya mnamo 2016, na wanachama wake wakaendesha kampeni ili kubakia na kutoka wakati huo huo ndani ya Muungano huo!

3- Kwa kuichunguza sera hiyo ya chama tawala cha conservative ambacho Cameron anakiongoza kuhusiana na kadhia ya kura ya maoni iliyotajwa, basi inaashiria kwamba Cameron alitarajia matokeo yake kutokuwa ya mwisho, kama vile kutoka sare, ili iwe ni jambo la kukubali au kukataa ili kuweko na mwanya wa marudio au kuyachukua matokeo hayo yasio ya mwisho kama nafasi kwa majadiliano mapya pamoja na EU. Ni kwa sababu hii ndio chama cha conservative chenyewe kilikuwa kikisimamia kampeni ili kubakia ndani ya Muungano pamoja na kampeni ya kujitoa kutokana nao. Kati ya kampeni zote hizi hakuna iliyokuwa makini kuhusu kubakia au kuondoka, mbali na kuwa zote mbili ziliikuwa na umakinifu kuhusu kura hiyo ya maoni inayo wakilisha njia ya kufikia maslahi ya ziada kutoka EU. Kwa sababu hiyo, inatarajiwa kuwa Uingereza itasitisha kuondoka kwa muda mfupi na kwa hakika huenda kukarefushwa hadi miaka kadhaa. Hiyo ni ikiwa itaondoka huku ikiwa mahiri katika matumizi ya mbinu chafu na uhadaifu. Na kuhsiana na kile kilicho wazi na dhahiri kutokana na maoni, na yale ambayo vyombo vya habari vimetangaza kwa njia ya taarifa; yote hayo yanafanya kusita kwa mujibu wa utekelezaji wa kura hiyo ya maoni kutarajiwa zaidi, bali hata zaidi ya hayo kama kupindua na kugeuza hatua kuhsiana na kura ya maamuzi yenye (30 Ramadhan 1437 H - 05/07/2016 M)] Mwisho wa nukuu.

Pili: Yanayojiri sasa yanazungumzia karibia yote tulio kwisha yasema kuhsiana na "mchezo wa kura ya maoni" na kucheleweshwa na kuzungushwa ili kufikia maslahi ya Uingereza, hata kama ni maovu. Haya yanathibitishwa kuititia kuyafahamu yafuatayo:

1- May amepokea kushindwa kukubwa katika bunge la House of Commons baada ya "makubaliano ya kujitoa Muungano wa Ulaya yaliyoafikiwa kwa idadi kubwa kukataliwa, katika kushindwa kukubwa kabisa

kwa serikali bungeni katika historia ya nchi hiyo ... Mnamo Jumatano Wabunge 432 walipiga kura kukataa makubaliano hayo," (Chanzo shirika la habari la BBC, 16/1/2019). Hii inamaanisha kuwa makubaliano hayo, ambayo yalitiwa saini ili kuitoa Uingereza nje ya Muungano wa Ulaya mnamo 29 Machi, hayatatekelezwa. Mazungumzo ya kujitoa hayakufta miondoko ya desturi ya chama tawala cha Conservative badala yake wanachama 118 wa Chama cha Conservative walipiga kura bungeni dhidi ya makubaliano ya waziri mkuu, na kijiungu na vyama vya upinzani. (Huku ni kushindwa kukubwa kabisa katika Bunge la Uingereza tangu 1924 ... matokeo yake ni kushindwa kubaya sana na bunge kwa serikali ya Uingereza katika enzi hizi za sasa ... (Chanzo: CNN Arabic 15/1/2019)".

2- Kiongozi wa Chama cha upinzani cha Uingereza cha Labour, Corbyn, alitangaza baada ya bunge kukataa kujitoa kwa ufalme huo kutoka katika Muungano wa Ulaya kwamba amewasilisha mswada wa kutokuwa na imani na serikali ya Theresa May ili ujadiliwe. Alisema: "Serikali hii imepoteza imani ya Baraza hili ... Nataka kujujulisha, Bwana Spika, kwamba nimewasilisha mswada wa kura ya kutokuwa na imani kwa ajili ya majadiliano ... Ninafuraha kuwa mapendekezo haya yatajadiliwa kesho" (Chanzo: RT Arabic, 15/1/2019), lakini matokeo ya kura hiyo yalimpendelea May kwa sababu wanachama 118 wa Chama cha Conservative walirudi kukiwigia kura dhidi ya upinzani, na wakazuia kura ya kutokuwa na imani juu ya May, na hivyo "Waziri Mkuu wa Uingereza Theresa May mnamo Jumatano, 16/1/2019 akaponea kushindwa katika Bunge la House of Commons kufuatia kufeli kwa mswada huo wa kutokuwa na imani juu ya serikali yake uliosalimishwa na Chama cha Upinzani cha Labour, baada ya kushindwa kwake juu ya makubaliano ya kujitoa kwa Uingereza (Brexit). Lakini serikali yake ilishinda imani kwa kura 325 dhidi ya 306, ambapo ilisitisha kufanyika kwa uchaguzi mkuu mpya. Hii ndio mara ya kwanza kuwepo na kura ya imani juu ya serikali katika Bunge la House of Commons kwa miaka 26. Mara moja viongozi wa upinzani waliitisha mkutano naye kwa ajili ya mazungumzo juu ya kujitoa kwa Uingereza (Brexit) na kuanzia mnamo Jumatano.

Matokeo ya kura ya Jumatano yalionyesha kuwa karibu Wabunge 100 wa Chama cha Conservative waliopiga kura Jumanne dhidi ya makubaliano ya kujiondoa kwa Uingereza (Brexit) walirudi mnamo Jumatano na kupiga kura dhidi ya mswada wa kutokuwa na imani dhidi ya serikali." (Chanzo: Agence France-Presse, mnamo 16/1/2019). Hivyo basi kuwa na fursa hadi Jumatatu, 21/1/2019) ili kuwasilisha "mpango mbadala", na yeze ana machaguo kadhaa, kama vile ahadi ya kurudi katika majadiliano jijini Brussels, au kuomba kuakhirisha kwa tarehe ya kujitoa kwa Uingereza (Brexit), iliopangwa kuwa 29 Machi 2019, au kujitoa pasi na makubaliano! Raisi wa Tume ya Ulaya alisema: "Natoa wito kwa Uingereza kufafanua nia zake haraka iwezekanavyo. Hakuna muda zaidi" (Chanzo: News site on 17/1/2019)

Endelea Uk..15

3- Hivyo basi, mchezo wa waamuzi wa Kiingereza uko wazi; badala ya kura ya kutokuwa na imani na May mnamo 16/1/2019, kwa sababu ya kufeli kwa mradi wake wa Brexit katika kura ya maamuzi ya mnamo 15/1/2019, May alishinda kura ya kuwa na imani ingawa kuanguka kwa mradi wake na kujishindia kwake imani ni kadhia mbili zanazo kinzana! Lakini endapo unajua ni kwa nini, inaongezea kizungumkuti zaidi!! Wabunge 118 wa Chama cha May walipiga kura dhidi ya mradi wa May, hivyo kuongeza sauti kwa upinzani uliopelekea kufeli kwa mradi wa May! Lakini wanachama hao 118 wa chama cha May walirudi na kupiga kura dhidi ya upinzani, yaani dhidi ya kura ya kutokuwa na imani na May, na hivyo May akashinda kura ya kuwa na imani na hakuanguka kwa kuanguka mradi wake!

4- Kwa kuelewa hilo la juu, ni wazi kuwa kura ya maoni ya 2016 ilidhamiria kuihalalishia Uingereza kuboresha masharti ya uhusiano mpya pamoja na Muungano wa Ulaya. Hii ndio sababu May aliwaruhusu wanachama 118 wa chama chake kupiga kura dhidi yake pamoja na upinzani ili kuupotosha upinzani na kuupa nguvu ili mradi wake wa Brexit ufeli! Lau angetaka kura ya maoni ya 2016 kubakia imara, hangeruhusu idadi hii ya chama chake kupiga kura dhidi yake, lakini pindi kura ya kutokuwa na imani ilipofanywa, idadi hiyo ilifanywa kupiga kura dhidi ya upinzani ili May aokoke! Hii ni ili May aendelee kuutishia Muungano wa Ulaya ili kupata manufaa na maslahi na kuweka masharti kwa ajili ya uhusiano mpya pamoja na Ulaya. Uingereza haiwezi kuondoka kwa hatima kutoka Ulaya kama ambavyo haiwezi kubakia pamoja na sheria za Muungano zilizopo kwa sasa. Kujitoa kwa hatima kuna athari kubwa katika mshikamano wa Waingereza wenyewe, hususan Scotland na vile vile Ireland Kaskazini, na hivyo basi inataka kubakia lakini kwa masharti yake, au ikiwa hakuna hiyari isipokuwa kuondoka, basi iwe na uwezo wa kupata maslahi kwa gharama ya Muungano huo!

5- Kwa upande wake, EU inaisihi UK “kufafanua nia zake” juu ya kujiondoa kwa Uingereza kutoka katika EU “haraka iwezekanavyo...” Alionya hatari ya kujiondoa kwa ghasia kwa kura hii.” (Chanzo: CNN Arabic 15/1/2019) Mwisho. Tayari tumeshataja katika makala yetu baada ya kura ya maoni ya 2016.

“Inaoneka Ulaya imeshatambua na kugundua michezo ya Uingereza na hivyo inataka kufanya mkataba usio rasmi ili kulinda maslahi yake juu ya msingi wa muundo wa Norway na Sweden kabla ya kuamua kufanya kazi pamoja na Kifungu cha 50 cha Mkataba wa Lisbon ili kuanza michakato ya kujitenga. Lakini, tofauti na Norway na Sweden, Uingereza inataka kuingia soko la Ulaya lakini iko dhidi ya matembezi huru ya watu, ambayo ilikuwa kadhia kuu kwa wapiga kura wa Kiingereza. Merkel aliuondoa kwa nguvu uwezekano huo kwani matembezi huru ya watu ni mojawapo ya uhuru ambao EU inautukuza pamoja na uhuru wa ubadilishanaji

bidhaa, huduma na rasilimali.

EU inauhisi ujanja wa Uingereza. Kwa hiyo, Raisi wa Tume ya Ulaya, Jean Claude Juncker, alisema: “Wacha niwe wazi kabisa, hatuvezi kuwa na majaribio ya kisiri ya kuiweka pemberi serikali ya Uingereza, ili yawe majadiliano ya siri, yasio rasmi” na akasema: “Nimetoa amri wazi kabisa kwa makamishna na wafanyakazi wote wa Tume; ni marufuku kuwepo majadiliano ya siri, hakuna majadiliano ya siri” (Chanzo: Evening Standard, 28/06/2016).

Merkel, Chansela wa Ujeruman, alielekeza ujumbe mkali jijini London aliposema: “Yeyote anayetaka kuondoka katika familia hii asitarajie kubwaga majukumu yake yote na kisha kudumisha maslahi yake” (Chanzo: (DPA 28/06/2016)] Mwisho wa nukuu.

6- Lakini, Uingereza haijagundua utambuzi wa Muungano wa Ulaya wa nia za Uingereza kwa umakinifu bali inaendelea na mchezo wa kura ya maoni iliyopita ya mnamo 15-16/1/2019 unaofutilia mbali kura ya maamuzi juu ya mradi wa Brexit. Hauondoi imani juu ya May, mhandisi wa mradi huo, bali unaufufua imani kwake ili kuanza mradi mpya na mpango mbadala! Hususan ili kutatua kadhia ya Ireland, katika hali ya kubakia au kuondoka kwake, na hivyo ndivyo ilivyokuwa, vyombo vyta habari viliripotia mipango ya May juu ya hili:

a- Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May, aliliambia bunge mnamo Jumatatu, 21/1/2019, (mpango wake “badala”, baada ya Wabunge kukataa makubaliano yake pamoja na Muungano wa Ulaya, juu ya “Brexit”. Uingereza itaondoka katika Muungano wa Ulaya mnamo 29 Machi, bila ya makubaliano, endapo Wabunge hawatawezi kuakhirisha tarehe ya kujiondoa, au kufikia mpango mbadala unaoridhisha Tume ya Ulaya vile vile ... Baada ya mipango ya May kukamilika juu ya jinsi ya kusonga mbele, Wabunge wataanzisha msururu wa marekebisho, yatakayo pigiwa kura, mnamo 29/1/2019. Mojawapo ya vipengee vyenye utata mkubwa katika makubaliano hayo kilicho kataliwa na bunge ni kifungu cha “kusimama nyuma”, dhamana ya usalama wa matembezi huru katika mipaka ya Ireland. Endapo Uingereza haitakubaliana na Muungano wa Ulaya juu ya mkataba wa muda mrefu wa biashara huru, gazeti la Sunday Times liliripoti kuwa May huenda akapendekeza mipangilio ya kujitenga pamoja na Dublin. Chanzo: AFP mnamo 21/1/2019) mwisho.

b- Gazeti la The Telegraph lilinukuu duru za kidiplomasia za EU ambazo hazikutajwa majina zikisema kuwa (matakwa ya May yanaendelea kupanuka kutoka kuunda mpaka wa muda wa kisheria hadi mpaka wa Ireland, ikiipatia Uingereza haki ya kujiondoa kipeke yake au kujifunga na mkataba wa biashara kabla ya 2021, ambayo inazuia utekelezwaji wa mipangilio maalumu kwa kadhia ya mipaka ya Ireland ... Chanzo: ... News of Libya on 21/1/2019)

c- (May alitangaza mnamo 21/1/2019 kuwa ananua

kurudi Brussels ili kujadili marekebisho ya makubaliano yake na viongozi wa Ulaya mwezi uliopita juu ya kadhia ya “kusimama nyuma”, ambayo yanapasa kuzuia kurudi katika kuasiwi mipaka imara kati ya Ireland mbili hizo baada ya Brexit. May alisema: “Nitaendelea kukutana na wenzangu wiki hii – ikiwemo maafisa wa chama cha Democratic Unionist Party cha Ireland Kaskazini – ili kuona namna tutakavyojifunga na majukumu yetu,” ikiwemo kuzuia kurudi kwa mipaka, “katika njia ambayo italeta usaidizi mpana iwezekanavyo” katika Bunge la House of Commons. Aliendelea: Nitaonyesha tamati ya mazungumzo haya kwa Muungano wa Ulaya.” Nchi nyenginezo 27 za Muungano wa Ulaya zinafuatilia kwa karibu hatua inayofuata itakayochukuliwa na May ... (Chanzo: France 24 / AFP mnamo 21/1/2019) Mwisho.

d- May alifichua baadhi ya mabadiliko katika msimamo wake juu ya Brexit. Waziri mkuu huyo aliahidi “kuonyesha mnyumbuko zaidi” katika mazungumzo pamoja na bunge hilo na kufikia matakwa ya chama cha upinzani cha Labour ya kuhakikisha haki za wafanyakazi wa Uingereza na kuondoa hofu yote kuhusu kurudi kwa mpangilio mikali ya ushuru wa forodha baina ya Ireland Kaskazini na Jamhuri ya Ireland. Imepangwa kuwa Theresa May alilikabidhi Bunge la Uingereza mpango mpya juu ya masharti ya kujiondoa kwa UK kutoka Muungano wa Ulaya, baada ya Bunge mnamo 15/1/2019 kukataa mpango wa kwanza ulioafikiwa kati ya serikali ya May na Brussels. Bunge la Uingereza litapiga kura juu ya mpango mpya mnamo 29/1/2019. (Chanzo: RT Arabic 21/1/2019).

7- Tamati ni kuwa Uingereza haina sifa ya kujitolea katika makubaliano yoyote, lakini mabadiliko na mabadiliko kupitia mchezo wa kura ya maoni, na ni mahiri, mwerevu na mjanja katika jambo hili ili kufikia maslahi yake maovu. Jana, kura ya maamuzi ya Uingereza iliidhinisha mradi wa Brexit na leo kura ya maaoni ya Uingereza imeidhinisha kutupilia mbali mradi wa Brexit! Hii ni ili kuutishia Muungano wa Ulaya kuleta marekebisho kwa mradi huo kwa gharama ya Muungano huo. Ingawa warasilimali Wamagharibi hawana vima vya kudumu, lakini Uingereza kupitia historia yake ya ukoloni imepata ujanja na uovu zaidi kushinda wengine. Uingereza haitaki kujiondoa kwa kabisa kutoka katika Muungano huo lakini inataka mpangilio mwengine sio wa kujiondoa wala wa kubakia! Yaani kuondoka katika Muungano huo na wakati huo huo kubakia ndani yake! Kwa hivyo iendelee kunufaika kutokana na mahusiano ya kifederali bila ya kutii sheria za Muungano huo, lakini isipokuwa lile tu lenye maslahi kwake. Na kama ilivyotajwa, na Chansela wa Ujeruman Angela Merkel, baada ya kura ya kwanza ya maoni na kuzuka kwa uakhirishaji wa Uingereza, alituma ujumbe wazi jijini London: “Yeyote anayetaka kuondoka katika familia asitarajie kubwaga majukumu yake yote na kisha kudumisha maslahi yake” (Chanzo: DPA 28/06/2016). Muungano wa Ulaya waweza kuifanya Uingereza kuteseka kutokana na matokeo endapo itasisitiza juu ya mradi wa Kwanza wa Brexit pasi na

kurekebisha vifungu vyake vyovoyote. Ni ima vikubaliwe na kutekelezwa na Uingereza au Uingereza ijiondoe kutoka kwa Muungano huo. Endapo EU itafanya hivi, Uingereza itakuwa imeanguka ndani ya uovu wa kazi yake; endapo itakubali masharti ya Uingereza hapo Uingereza itaipa maamrisho hadi iimalize pasi na yenewe kujua!

Hii ndio hali ya mataifa yanayo tabanni usekula kwa dola na mfumo wa kirasilimali. Yanachimbiana mashimo marefu ambapo kundi mionganii mwao au wote hutumbukia ndani yake. Hawana vima vinavyo wazuia au maadili yanayo wakataza, bali vita mionganii mwao ni vikali kama yalivyo mataifa mengine yasiyojifunga na hukumu ya Mwenyezi Mungu.

بَأْسُهُمْ بِئْنَهُمْ شَدِيدٌ تَحْسَبُهُمْ جَمِيعاً وَقُلُوبُهُمْ شَنِيْنِ ذِكْرٍ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ
“Wao kwa wao vita vyao ni vikali. Utawadhania kuwa wako pamoja, kumbe nyoyo zao ni mbali mbali. Hayo ni kwa kuwa wao ni watu wasio na akili.” [Al-Hashr: 14].

Ulimwengu huu hautakuwa mahali pazuri na mateso yanayouzunguka hayataondoka isipokuwa kwa sheria ya Mwenyezi Mungu isimamishwe katika utawala kupitia kusimamishwa Khilafah Rashida. Haitaeneza tu uadilifu na kheri katika miji yake, bali itasambaza uadilifu na kheri hii ulimwengu mzima kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

وَلَنَغْلَمَنَّ نَبَاهُ بَعْدَ حِينِ
“Na bila ya shaka mtajua habari zake baada ya muda.”
[Sad: 88]

**19 Jumada Al-Awwal 1440 H
25/1/2019 M**